**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

***Dar es Salam***
***21 Julai, 2026***

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA KUSHIRIKI KATIKA MKUTANO MKUU MAALUM WA AU KUHUSU AFYA, NCHINI GHANA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo tarehe 21 Julai, 2026, anaondoka nchini kuelekea Jamhuri ya Ghana, kwa ziara ya kikazi ya siku moja.

Rais Dkt. Samia atashiriki Mkutano Mkuu Maalum wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu Afya, utakaofanyika tarehe 22 Julai, 2026 jijini Accra, nchini humo.

Mkutano huo wenye kaulimbiu: ***"Kuendeleza Haki, Usawa na Huduma za Afya kwa Wote,"*** utajadili hatua za pamoja za kutokomeza magonjwa ya UKIMWI na Kifua Kikuu, kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika vya wajawazito na watoto, pamoja na kuimarisha mifumo ya afya barani Afrika.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu